# TARATIBU ZA UTOAJI WA LESENI ZA JUMLA ZA BIASHARA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

**(Imetolewa na kifungu 11(1) kwa sheria ya leseni za biashara ya namba 25 ya 1972) Upatikanaji wa Leseni ya Biashara.**

1. Chukua fomu ya maombi ya biashara (TFN 21 Business License Application form ) inayopatikana kitengo cha biashara
2. Soma kwa makini na jaza kila kipengele kwenye fomu ambacho kinahusiana na biashara yako. Ni muhimu kusoma melezezo yote yaliyoko kwenye fomu kabla hujaondoka Ofisi ya Biashara ili uweze kupata maelekezo kwenye vipengele ambavyo hujavielewa.
3. Ukaguzi wa Maafisa Mipango miji, Afya na Biashara utafanyika kwa baadhi ya ya biashara mfano bucha, nyumba za kulala wageni, hoteli na migahawa, mashine za kukoboa na kusaga nafaka na gereji.
   - ➢ Afisa Afya atakagua na kutoa ushauri wa kiafya kulingana na aina ya biashara inayoombwa.
   - ➢ Afisa Biashara atakagua fomu ya maombi ya leseni kwa kuangalia leseni ya biashara inayoombwa kama inakubalika kwa mujibu wa sheria ya leseni husika na kama taratibu zote zimezingatiwa.
4. Muombaji atatakiwa kuwasilisha fomu ya maombi ya leseni ya biashara iliyojazwa kikamilifu ikiwa imeambatanishwa na hati ya uthibitisho wa mlipa kodi yaani (Tax Clearance Certificate) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na hati nyingine zinazohusika kutegemeana na aina ya biashara

### Utoaji wa Leseni

1. Mfanyabiashara huandaliwa hati ya malipo (Bill) kulingana na Biashara yake na atalipia ada ya leseni anayopaswa kulipa katika tawi la benki ya NMB kisha anaandaliwa leseni yake.
2. Muda wa leseni ni miezi 12 tangu leseni inapolipiwa. Baada ya leseni kwisha muda wake wa kutumika, mfanyabiashara anapewa siku ishirini na moja (21) za kuhuisha leseni yake bila adhabu (penati), akichelewa atalipia na ada ya leseni pamoja na adhabu (penati) ambayo huanza kwa asilimia ishirini na tano (25%) na huenda ikiongezeka kwa asilimia mbili (2%) kila mwezi.
3. Leseni za ushauri na utaalamu maalum pia hutolewa kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri na utaalamu ambapo mhusika ni lazima awe amesomea fani aliyoomba au kuajiri mtu mwenye sifa zinazotakiwa. Huduma hiyo ni kama maabara, wakandarasi mbali mbali, uuzaji madawa, upuliziaji wa madawa ya kuua wadudu (fumigation), huduma za hospitali n.k. Utoaji wa huduma hizi mhusika anatakiwa awe amesajiliwa na Mamlaka au Bodi za udhibiti wa taaluma husika. Huduma/ Utaalamu wa Mamlaka/Bodi husika na kama ilivyoainishwa hapa chini;-
   - Ukandarasi wa ujenzi- Contractors Registration Board (CRB)
   - Utengenezaji Mahesabu/Ukaguzi wa hesabu- National Board of auditors and Accountant (NBAA)
   - Upuliziaji wa dawa za kuua wadudu kwenye mashamba,majengo- Tropical Pesticides Research Institute (TPRI)
   - Uwakili- Tanganyika Law Society (TLS)
   - Udaktari- Medical Council of Tanzania (MCT)
   - Uuzaji wa Madawa, chakula na vipodozi- Tanzania Food and Drugs Authority (TFDA)
   - Uuzaji wa dawa za binadamu- Tanzania Pharmacy Council (TPC)
   - Uuzaji wa dawa za Kilimo na Mifugo- Tanzania Veterinary Council (TVC)
4. Ni kosa kisheria kufanya biashara bila kuwa na leseni. Adhabu Yake ni kulipia faini ya shilingi 50,000 – 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote viwili.

### Masharti ya Kuomba na Kupewa Leseni za Biashara

1. Mfanyabiashara anapaswa awe na hati ya usajili iwapo anatumia jina la biashara (Certificate of Registration or Incorporation)
2. Kama ni kampuni mwombaji awe na "Memorandum and Article of Association" ambazo zinaonyesha kuwa kampuni imeruhusiwa kufanya biashara anayoiomba.
3. Awe na mahali/ eneo linalokubalika kwa aina ya biashara anayoiomba na isiwe vibanda vilivyopo kando kando ya barabara.
4. Mfanyabishara aje na (Tax Clearance) ambayo inatolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
5. Masharti mengine ya kupata Leseni hutegemea aina ya biashara mtu anayotaka kuanzisha mfano Mgahawa inabidi afuate taratibu zote za afya na kupima wafanyakazi wake.
6. Hati ya Utaalamu (Professional Certifucates) kwa biashara zote za kitaalamu.

### Malipo

Kiwango cha ada ya leseni kinatofautina kulingana na aina ya biashara husika.Baada ya ulipaji wa ada hiyo mfanyabiashara atapatiwa stakabadhi kwa malipo halali ya fedha yake

Kuhuisha (Kurenew) leseni za biashara

Mfanyabiashara anayehuisha leseni anatakiwa aje na nakala ya leseni iliyoisha muda wake pamoja na kibali cha mlipa kodi (Tax Clearence Certificate) kutoka Malmlaka ya mapato Tanzania (TRA).

### Wajibu wa Mfanyabiashara

1. Kulipia kila mwaka leseni ya biashara yake kwa mujibu wa sharia
2. Ni jukumu la kila mfanyabishara kumiliki leseni katika eneo lake la biashara na kuiweka mahali pa wazi ili kuonekana kwa urahisi.

### Faida za Mfanyabiashara kuwa na leseni ni pamoja na;

1. Kutambulika kama mfanya biashara halali
2. Husaidia kupata mikopo mbalimbali
3. Husaidia kupata fursa mbalimbali za kibiashara
4. Kuchangia katika uchumi wa Taifa (Ada)
5. Kuepuka usumbufu wa kufungiwa biashara kwa kutokuwa na leseni halali.

***Muhimu:***- Ndugu mfanyabiashara, unapofunga biashara unatakiwa kutoa taarifa kwa maandishi kwa wakati kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI
VEGA
Volunteers for Economic Growth Alliance
iesc
THE NONPROFIT THAT MEANS BUSINESS

# TARATIBU ZA UTOAJI WA LESENI ZA VILEO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

1. Ujazaji wa fomu ya maombi ya leseni za vileo ni kwa Mujibu wa Sheria ya Vileo Na 10:2:1968 marekbisho ya Mwaka 1971 na 1998) ambazo zinpatikana kitengo cha biashara ambazo pia zinapatikana Ofisi za Biashara Wilaya.
2. Leseni za vileo, maombi hutumwa kwa Bodi ya Vileo kila mwezi wa tatu ( Machi) na mwezi wa tisa (Septemba) kila mwaka kabla ya leseni kuisha muda wake.

- Kwa kuwa biashara hii inahitaji kuhusisha wataalumu wa kada mbalimbali , Maafisa wa Mkurugenzi kama vile Afisa Afya, Afisa Biashara pamoja na Afisa Mpango Miji, watafanya ukaguzi wa eneo la biashara.
- Afisa Afya anakagua na kutoa ushauri wa kiafya.
- Afisa Biashara anakagua fomu ya maombi ya leseni kwa kuangalia leseni ya biashara inayoombwa kama inakubalika kwa mujibu wa sheria ya leseni husika na kama taratibu zote zimezingatiwa.
- Afisa mipango Miji atakagua eneo la biashara kama limetengwa au linafaa kufanya biashara inayoombewa

3. Baada ya kukaguliwa na wataalmu hao, ikiwa mwombaji atakidhi vigezo, atatolewa hati ya malipo ya ada ya leseni kwa ajili ya kwenda kulipia benki na baadae kupatiwa leseni yake

**Uhai wa leseni**

Leseni ya vileo inadumu kwa miezi sita kutegemeana na mwezi alichukua, mara baada ya kuisha muda wake, mfanyabiashara anapewa siku ishirini na moja (21) za kulipia leseni yake bila faini akichelewa hulazimika kulipia faini ambayo huanzia asilimia ishirini na tano (25%) na huongezeka kwa asilimia mbili (2%) kila mwezi.

**Malipo ya ada ya leseni**

Kiwango cha ada ya leseni kinatofautina kulingana na ukubwa wa biashara ya vileo .Baada ya ulipaji wa ada hiyo mfanyabiashara atapatiwa stakabadhi kwa malipo halali ya fedha yake.

Angalia Jedwali la viwango vya ada za Leseni za vileo kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Retailers On Licence (Baa) | - 30,000 hadi 40,000 |
| 2. | Retailers Off Licence (Grocery) | - 20,000 hadi 30,000 |
| 3. | Wholesale (Jumla) | - 10,000 hadi 20,000 |
| 4. | Members Club Licence ( Klabu wanachama) | - 10,000 hadi 20,000 |
| 5. | Restaurant & Retailers On Licence | - 30,000 hadi 40,000 |
| 6. | Temporary Licence (Leseni ya muda) | - 7,000 hadi 15,000 |
| 7. | Hotel Licence (Leseni ya hoteli) | - 30,000 hadi 40,000 |
| 8. | Retailers Off Licence non-spirituous | - 10,000 hadi 15,000 |
| 9. | Retailers On Licence non-spirituous (Stores) | - 10,000 hadi 15,000 |

- Mamlaka ya Vileo itaamua kiwango cha ada kitakachotozwa kati ya kiwango cha chini na kile cha kima cha juu. Viwango vinavyotumika kwa sasa na Halmashauri ya Wilaya ni vile vya kima cha juu kwa kila aina ya leseni.

**Kuhuisha (ku-renew) leseni za biashara**

Mfanyabiashara anayehuisha leseni anatakiwa aje na nakala ya Leseni iliyoisha muda wake pamoja na kibali cha mlipa kodi (Tax Clearence Certificate) kutoka TRA.
Masharti ya utumiaji
Leseni za vileo zina masharti mengi ikiwa ni pamoja na kutouza kilevi kwa watoto . Masharti mengine ni muda wa kuuza pombe na kelele za muziki. Muda wa kuuza pombe ni kama ifuatavyo:-

**BAA (Retailers On licence)**

(a) Maeneo ya mjini:
- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 12.00 jioni hadi saa 5.00 usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 6.00 usiku.

(b) Maeneo ya vijijini:
- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 9.00 alasiri hadi saa 2.00 usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 8.00 mchana hadi saa 5.00 usiku.

GROCERY (Retailers off Licence)
- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 2.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 3.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni.

POMBE ZA ASILI (Local Liquour Licence)
- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 6.00 mchana hadi saa 5.usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 5.00 usiku.

- Mfanyabiashara yeyote wa pombe anapaswa kufuata utaratibu huu ambao ni wa kisheria.

**Wajibu wa mfanyabiashara**

1 Kulipia kila mwaka lesseni ya biashara yako kwa mujibu wa sharia.
2 Ni jukumu la kila mfanyabiashara kumiliki leseni katika eneo lake la biashara na kuiweka mahala pa wazi ili kuonekana kwa urahisi wakati wa ukaguzi.
3 Ni kosa kisheria kufanya biashara bila kuwa na leseni. Adhabu Yake ni kulipia shilingi 50,000 – 100,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote viwili. Hata hivyo viwango hivi vya adhabu vinaweza kubalishwa na Serikali.

**Faida za mfanyabiashara kuwa na leseni ni pamoja na:**

6. Kutambulika kama mfanya bihashara halali
7. Husaidia kupata fursa mbalimbali za kibiashara
8. Kuchangia katika uchumi wa Taifa (Ada)
9. Kuepuka usumbufu wa kufungiwa biashara kwa kutokuwa na leseni halali na kushitakiwa kwa mujibu wa Sheria Kanuni na Taratibu za Serikali

Muhimu:- Ndugu mfanyabiashara, unapofunga biashara ya vileo unatakiwa kutoa taarifa kwa maandishi kwa wakati kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

IMEANDALIWA NA: -
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KYELA